# RIPOTI YA UWEKEZAJI TANZANIA 2024

## UWEKEZAJI WA MITAJI BINAFSI KUTOKA NJE

# MUHTASARI

# RIPOTI YA UWEKEZAJI TANZANIA 2024

## UWEKEZAJI WA MITAJI BINAFSI KUTOKA NJE

# MUHTASARI

# UTANGULIZI

Ripoti ya uwekezaji Tanzania ya mwaka 2024 inatoa tathmini ya kina kuhusu mchanganuo wa mitaji binafsi ya kigeni iliyopokelewa nchini kutoka kwa wawekezaji wa kigeni kupitia uwekezaji mkubwa wa moja kwa moja – kuanzia asilimia 10 ya hisa na zaidi (FDI), uwekezaji mdogo - chini ya asilimia 10 (PI), na uwekezaji mwingine – unaotokana na mikopo kutoka kwa wasio wanahisa kwenye makampuni yaliyowekeza nchini (OI). Ripoti inaonesha kuwa uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara licha ya changamoto za kiuchumi zinazoikabili dunia, hususan, migogoro ya kisiasa inayoendelea duniani. Ripoti inajikita katika kuainisha vyanzo na sekta za uwekezaji.

Ripoti hii imeandaliwa kwa ushirikiano wa taasisi tatu ambazo ni Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Utayarishaji wake unaongozwa na muundo wa ngazi tatu, yaani Kamati ya Wakuu wa Taasisi (Chief Executive Committee), Kamati ya Uongozi (Steering Committee) inayoratibu uandaaji wa ripoti, na Kamati ya Wataalam (Technical Committee) ambayo inahusika na ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi, na uandishi wa ripoti.

Ripoti hii inaainisha vyanzo, mienendo, vichocheo, na umuhimu wa uwekezaji wa kigeni kwa uchumi wa Tanzania. Aidha, madhumuni mahsusi ya ripoti hii ni pamoja na:

- Kukusanya na kuchambua takwimu za uwekezaji wa mitaji binafsi kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kupima na kuendeleza

mikakati ya kujitangaza, kuboresha takwimu za mizania ya urari wa malipo pamoja na kuainisha hali ya uwekezaji wa kimataifa nchini (international investment position);

- Kupendekeza sera muafaka na mikakati ya kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.
- Kuainisha fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo nchini kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi.

Kitabu hiki kinatoa muhtsari wa matokeo muhimu yaliyojitokeza kwenye utafiti uliofanywa na kukusanya takwimu za mwaka 2023. Utafiti ulihusisha makampuni yaliyochaguliwa kwa kuzingatia vigezo vya kitakwimu (sampuli), ambapo makampuni 541 yenye uwekezaji kutoka nje yaliyohusishwa na mwitikio ulikuwa wa kuridhisha, wa wastani wa asilimia 84.

Ripoti kamili (Tanzania Investment Report 2024) inapatikana katika tovuti za Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

# MATOKEO MUHIMU

## Uwekezaji wa Mitaji Binafsi Kutoka Nje

Mwaka 2023, uwekezaji wa mitaji binafsi kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 3.9 na kufikia dola za Marekani milioni 23,042.5. Ukuaji huu umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka tangu mwaka 2019 (Jedwali 1). Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na ongezeko la asilimia 5.8 la uwekezaji wa moja kwa moja (FDI), hususan kutoka kwenye faida zilizorudishwa pamoja na mikopo kutoka kwa wanahisa wakubwa. Matokeo haya yanaashiria imani waliyo nayo wawekezaji juu ya uimara wa uchumi wetu kutokana na mazingira bora ya biashara na uwekezaji.

### Jedwali 1: Uwekezaji wa Mitaji Binafsi Kutoka Nje, 2019 – 2023

Dola za Marekani Milioni


| Aina | Uingiaji | | | | | Limbikizo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
| Uwekezaji wa moja kwa moja | 1,217.2 | 943.8 | 1,190.5 | 1,437.6 | 1,648.9 | 14,762.9 | 15,612.6 | 15,741.1 | 18,095.8 | 19,139.6 |
| Hisa na Uwekezaji wa wanahisa | 1,096.2 | 903.0 | 961.6 | 1,312.3 | 938.4 | 8,684.2 | 9,548.6 | 10,201.0 | 9,899.3 | 10,573.4 |
| Hisa na Uwekeza wa Wanahisa isipokuwa mapato ya faida | 773.4 | 327.0 | 392.5 | 492.3 | 213.5 | 9,016.0 | 9,368.2 | 5,807.4 | 6,399.4 | 6,324.2 |
| Uwekezaji wa Mapato ya Faida | 322.8 | 576.0 | 569.1 | 820.0 | 724.9 | -331.8 | 180.4 | 4,393.6 | 3,499.9 | 4,249.2 |
| Mikopo | 121.1 | 40.8 | 228.9 | 125.3 | 710.5 | 6,078.7 | 6,064.0 | 5,540.1 | 8,196.4 | 8,566.2 |
| ya muda mrefu | 35.0 | 94.6 | 173.7 | -25.1 | 558.9 | 5,540.2 | 5,581.6 | 5,196.1 | 6,294.5 | 7,508.8 |
| ya muda mfupi | 86.1 | -53.9 | 55.2 | 150.4 | 151.6 | 538.5 | 482.3 | 343.9 | 1,902.0 | 1,057.4 |
| Uwekezaji mdogo wa moja kwa moja | 5.5 | 1.8 | 4.9 | 0.2 | 1.4 | 104.6 | 124.8 | 126.8 | 195.8 | 204.3 |
| Uwekezaji mwingine | 17.3 | -85.5 | -8.6 | 308.1 | 44.5 | 2,810.0 | 2,724.5 | 3,056.5 | 3,890.8 | 3,698.6 |
| Mikopo ya muda mrefu | 1.3 | -32.7 | -12.9 | 190.3 | -142.2 | 2,189.7 | 2,127.4 | 2,236.9 | 2,730.5 | 2,433.0 |
| Mikopo ya muda mfupi | -51.1 | -3.0 | -15.5 | 0.4 | -47.9 | 35.0 | 50.9 | 185.8 | 154.3 | 97.8 |
| Biashara malipo ya awali | 66.3 | -47.4 | 16.5 | 117.1 | 234.4 | 350.2 | 301.5 | 610.3 | 996.5 | 1,155.4 |
| Amana na sarafu | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Hisa nyinginezo | 0.8 | -2.5 | 3.3 | 0.3 | 0.2 | 235.1 | 244.7 | 23.5 | 9.4 | 12.3 |
| Jumla ya Uwekezaji Binafsi wa Kigeni | 1,240.0 | 860.1 | 1,186.8 | 1,745.8 | 1,694.8 | 17,677.5 | 18,461.9 | 18,924.3 | 22,182.4 | 23,042.5 |

*Maelezo: Uwekezaji Mwingine (OI) unahusisha aina yoyote ya uwekezaji ambao haujajumuishwa ndani ya Uwekezaji wa moja kwa moja (FDI) na Uwekezaji wa Hisa (PI).*

## 1. Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje (FDI)

**Kielelezo 1: Uwekezaji wa Moja kwa Moja (FDI), 2019 – 2023**

Dola za Marekani Milioni





Uwekezaji wa moja kwa moja (FDI) umeendelea kuongezeka katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, licha ya kupungua mwaka 2020 kufuatia athari za janga la UVIKO-19. Mwaka 2023, uwekezaji wa moja kwa moja uliongezeka kwa asilimia 14.7 na kufikia dola za Marekani milioni 1,648.9 ikilinganishwa na mwaka 2022 (Kielelezo 1).

Ukuaji huu ulitokana hasa na ongezeko kubwa la mikopo kutoka kwa wanahisa, ambapo mchango wake kwenye jumla ya mitaji ya moja kwa moja uliongezeka hadi asilimia 43.1 kutoka asilimia 8.7 mwaka ulipita. Ongezeko hili linaonesha juhudi za serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, sambamba na mageuzi ya kimuundo na uendelezaji wa huduma za kidijitali katika sekta mbalimbali.

## 1.1 Ufadhili wa Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje (FDI)

**Kielelezo 2: Vyanzo vya Mitaji ya FDI, 2019 – 2023**

Asilimia




Katika mwaka 2023, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ulifanyika zaidi kupitia mikopo ya muda mrefu na faida zilizorejeshwa kutoka kwenye uwekezaji. Aidha, kulikuwa na mabadiliko ya vyanzo vya mitaji kutoka kwenye uwekezaji wa wanahisa, na urejeshwaji wa faida kwenda kwenye mikopo ya muda mrefu kutoka kwa wanahisa (Kielelezo 2). Mabadiliko haya ni kielelezo kuwa wawekezaji wana imani na ukuaji wa uchumi, sambamba na jitihada za uboreshaji mazingira ya uwekezaji.


## 1.2 Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi

Mwaka 2023, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ulijikita zaidi katika shughuli za uchimbaji madini na uchorongaji, uzalishaji bidhaa viwandani, fedha na bima, pamoja na habari na mawasiliano, ambapo

kwa pamoja zilichangia asilimia 82.4 ya jumla ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (Kielelezo 3). Aidha, shughuli hizi zilikuwa miongoni mwa shughuli tano za kiuchumi zilizokuwa kwa kasi zaidi katika mwaka 2023, isipokuwa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani. Uwekezaji katika shughuli za habari na mawasiliano uliongezeka zaidi ya mara mbili hadi dola za Marekani milioni 198, ukichochewa na mahitaji makubwa ya huduma za mtandao na miamala ya pesa kupitia simu za kiganjani.

**Kielelezo 3: Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi, 2019 – 2023**

Asilimia



Uwekezaji wa mitaji katika shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani uliongezeka zaidi ya mara mbili hadi kufikia dola za Marekani milioni 361 mwaka 2023, kutokana na kuimarika kwa shughuli za uzalishaji licha ya changamoto za ukuaji wa uchumi duniani, sanjari na juhudi za serikali za kuimarisha viwanda. Katika shughuli za fedha na bima, uwekezaji wa mitaji uliongezeka kwa asilimia 12.3 na kufikia dola za Marekani milioni 267.6, ukichangiwa zaidi na ongezeko la mikopo na uboreshwaji wa huduma na bidhaa za kifedha.



**Kiwanda cha Mbolea cha ITRACOM**



**Shughuli za Fedha na Bima**

Wakati huo huo, shughuli za uchimbaji madini na uchorongaji, ambazo zilikua mchangiaji mkubwa wa mitaji ya moja kwa moja kutoka nje, zilipokea dola za Marekani milioni 532.5, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 847.1 mwaka 2022. Kushuka huku kulisababishwa na ulipaji wa mikopo na hasara zilizopatikana na baadhi ya makumpuni yaliyo katika hatua za awali za kutafuta madini (exploration). Kumekuwa na ongezeko kubwa la mitaji ya moja kwa moja kutoka nje katika shughuli za kilimo katika mwaka 2023, ikiashiria mwitikio wa juhudi za serikali za kuboresha sekta hii, ikiwa ni pamoja na ongezeko la bajeti kwa huduma za ugani, utoaji wa

mbegu bora, uboreshaji wa skimu za umwagiliaji na upatikanaji wa mikopo.



Shughuli za Uchimbaji Madini




Shughuli za Kilimo

## 1.3 Vyanzo vya Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje

### Kielelezo 4: : Nchi Kumi Zinazoongoza kwa FDI, 2021 – 2023

Dola za Marekani Milioni




Mwaka 2023, nchi zilizoongoza kwa uwekezaji wa moja kwa moja ni Mauritius, Australia, Uingereza, Barbados, Uholanzi, na Afrika Kusini. Nchi kumi zilizoongoza zilichangia asilimia 64.7 ya FDI (Kielelezo 4). Mabadiliko makubwa yalionekana katika Visiwa vya Cayman, Australia, na Uingereza, kufuatia mabadiliko ya umiliki wa hisa katika kampuni zinazojihusisha na shughuli za uchimbaji madini na uchorongaji.

Kwa upande wa limbikizo, orodha ya nchi kumi kwa ukubwa wa uwekezaji zilibaki takriban zile zile, huku Uingereza ikiendelea kuongoza kwa dola za Marekani milioni 5,152.6 mwaka 2023. Nchi nyingine zilizokuwa na uwekezaji mkubwa ni pamoja na Norway, Mauritius, na Uholanzi (Kielelezo 5).

**Kielelezo 5: Nchi Kumi Zilizoongoza Limbikizo la FDI, 2022 na 2023**


Dola za Marekani Milioni



## 1.4 Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kikanda na Makundi ya Kiuchumi

**Kielelezo 6: Uwekezaji wa FDI Kikanda na Makundi ya Kiuchumi, 2019 – 2023**

Asilimia




Nchi za Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) ziliendelea kuongoza, zikichangia dola za Marekani milioni 698.7 mwaka 2023, sawa na asilimia 42 ya uwekezaji wote wa moja kwa moja. Nchi zilizochangia zaidi katika kundi hili ni Australia, Uingereza, na Uholanzi, ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 74.2 ya jumla ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka OECD. Kanda ya SADC ilishika nafasi ya pili, ambapo uwekezaji uliongezeka zaidi ya mara mbili kufikia dola za Marekani milioni 430.9 mwaka 2023. Mauritius na Afrika Kusini zilichangia sehemu kubwa katika kundi hili. Kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Kenya iliongoza kwa zaidi ya asilimia 98 katika kundi hili (Kielelezo 6).

## 2. Mchango wa Uwekezaji Mdogo (PI) umeendelea kuwa mdogo, licha ya kuongezeka

Mwaka 2023, uwekezaji wa wanahisa chini ya asilimia kumi (portfolio investment) uliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1.4, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 0.2 mwaka 2022. Ongezeko hili linaashiria kuendelea kuimarika kwa uwekezaji kwenye dhamana za masoko ya mitaji. Takwimu kutoka soko la hisa la Dar es Salaam (DSE) zinaonesha kuwa thamani ya soko (market capitalization) ilifikia dola za Marekani bilioni 5.9 mwaka 2023. Licha ya ongezeko hili, uwekezaji katika masoko ya mitaji bado ni mdogo.

## 3. Uwekezaji Mwingine (OI)

Uwekezaji mwingine ni uwekezaji unaotokana na mikopo binafsi ya nje kutoka kwa wasio wanahisa (Other Investments). Uwekezaji wa aina hii ulipungua kwa kiasi kikubwa hadi kufikia dola za Marekani milioni 44.5 mwaka 2023, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 308.1 mwaka 2022. Kupungua huku kunatokana na ongezeko la urejeshaji wa madeni, hususan katika shughuli za fedha na bima, ikilinganishwa na upokeaji wa mikopo mipya. Hata hivyo, mikopo ya kibiashara na malipo ya awali yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 234.4 mwaka 2023, kutoka dola Marekani milioni 117.1 mwaka 2022 (Jedwali 2). Uwekezaji huu ulikuwa mkubwa zaidi kwenye shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani, pamoja na uchimbaji madini na uchorongaji.

## Jedwali 2: Uwekezaji Mwingine, 2019 – 2023


Dola za Marekani Milioni

| | Uingiaji | | | | | Limbikizo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
| Mikopo | -49.9 | -35.6 | -28.4 | 190.7 | -190.1 | 2,224.7 | 2,178.3 | 2,422.7 | 2,611.6 | 2,530.9 |
| ya muda mrefu | 1.3 | -32.7 | -12.9 | 190.3 | -142.2 | 2,189.7 | 2,127.4 | 2,236.9 | 2,425.8 | 2,433.0 |
| ya muda mfupi | -51.1 | -3.0 | -15.5 | 0.4 | -47.9 | 35.0 | 50.9 | 185.8 | 185.8 | 97.8 |
| Mikopo ya kibiashara na malipo ya awali | 66.3 | -47.4 | 16.5 | 117.1 | 234.4 | 350.2 | 301.5 | 610.3 | 725.8 | 1,155.4 |
| Hisa nyinginezo | 0.8 | -2.5 | 3.3 | 0.3 | 0.2 | 235.1 | 244.7 | 23.5 | 34.4 | 12.3 |
| Uwekezaji mwingine | 17.3 | -85.5 | -8.6 | 308.1 | 44.5 | 2,810.0 | 2,724.5 | 3,056.5 | 3,371.8 | 3,698.6 |

## 4. Faida

### Kielelezo 7: Faida na Gawio, 2021 – 2023

Dola za Marekani Milioni



Mwaka 2023, faida baada ya kodi ilikuwa dola za Marekani milioni 1,806.3, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,057.3 mwaka 2022. Shughuli zilizoongoza kwa faida ni fedha na bima, uzalishaji bidhaa viwandani, pamoja na habari na mawasiliano. Faida zilizorejeshwa kwenye kampuni zilipungua kwa asilimia 28.1 na kufikia dola za Marekani milioni 1,120.5, sambamba na kupungua kwa faida baada ya kodi na malipo makubwa ya gawio kwa wanahisa (Kielelezo 7). Aidha, gawio kwa wanahisa lililotangazwa (Dividend declared) liliongezeka hadi dola za Marekani milioni 685.8 kutoka dola za Marekani milioni 460.8 mwaka 2022.

# MWELEKEO WA UWEKEZAJI TANZANIA

## Mazingira ya Kiuchumi

Mwaka 2024, uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kuwa imara, kutokana na ukuaji mzuri wa mwaka 2023, licha ya changamoto za kiuchumi duniani. Pato Halisi la Taifa (GDP) linatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4, likichochewa na shughuli za kilimo, utalii, na uzalishaji bidhaa viwandani, huku miradi mikubwa ya miundombinu kama Reli ya Kisasa (SGR) na Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere ikiendelea kuchangia ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki chini ya asilimia 5, kutokana na uwepo wa akiba ya kutosha ya chakula, uboreshaji wa shughuli za usafiri, na utekelezaji wa sera madhubuti za kifedha na bajeti.

## Mikakati ya Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji

Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kupitia mikakati mahsusi, ikiwemo:

i. **Kuimarisha huduma na miundombinu:** Uboreshaji wa Vituo vya Pamoja vya huduma kwa wawekezaji na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Ushirika (Corporate Strategic Plan) wa kipindi cha mwaka 2023/24 hadi 2027/28.

ii. **Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi:** Ushiriki wa sekta binafsi unaendelea kuimarishwa kupitia Kampeni ya Kitaifa ya Kukuza Uwekezaji (NIPC).

iii. **Kuimarisha uwekezaji jumuishi:** Kuendeleza mashamba makubwa ya Mkulazi na Uvinza, pamoja na kuanzisha minada ya mazao kwa njia ya mtandao ambayo imeongeza tija na motisha kwa wawekezaji.

## Hitimisho

Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 14.7 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,648.9 mwaka 2023, ukiongozwa na shughuli za uchimbaji madini na uchorongaji, fedha na bima, habari na mawasiliano, na uzalishaji bidhaa viwandani. Kuongezeka huku kunatokana na jitihada kubwa zinazofanywa na serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha huduma za kidijitali na kuimarisha ushirikiano baina ya sekta za umma na binafsi kwa ukuaji endelevu wa uchumi.






**KWA MAELEZO ZAIDI, TAFADHALI TEMBELEA TOVUTI ZETU**

| TIC | BOT | NBS |
|---|---|---|
| www.tic.co.tz | www.bot.go.tz | www.nbs.go.tz |